

## **MRADI WA UBORESHAJI WA RELI YA KATI –TIRP**

### **1. TAARIFA ZA MRADI**

Mradi umelenga kufanya ukarabati wa relii liyopo kwa kipande cha Dar es Salaam – Isaka (Km 970) ili kuinua uwezo wa kubeba mzigoto ka chini ya tani 13.5 za uzito wa ekseli hadi tani 18.5 kwa kufanyayafuatayo:-

- Kutandika upya njia za reli zenyenye uzani wa paundi 80 kwa urefu wa kilometra 335.
- Kufanya ukarabati wa njia ya reli kwa urefu wa kilometra 555.
- Kufanya ukarabati makalavati na madaraja 393
- Kuboresha mfumo wa mawasiliano
- Ukarabati wa vituo vya kupakia na kupakua mizigo vya bandari ya Dar es Salaam, Ilala na Bandari Kavu ya Isaka.
- Ununuzi wa mitambo ya ukarabati wa njia

Inakadiriwa mataruma 566850, tani 30719 za reli pamoja na viungio vingine vitatumika katika ukarabati wa njia ya reli.

Sambamba na hilo kuititia mradi huu tutaweza kununua vichwa vitatu vya treni (vipyta) na mabehewa mapya 44 yamizigo, pia mradi kutakarabati vichwa viwili vya treni

### **2. YALIYOKWISHAKUFANYIKA**

Mradi huu una jumla ya mikataba 63 na tayari tumesha saini jumla ya mikataba 48 kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini

AinayaMkataba	Idadi	Iliyokwishaanza/Sainiwa
Ushauri/Consultancy	42	35
UnunuziwaVifaa/Goods	14	07
Ujenzi/Works	05	05
IsiyoyaKiushauri/Non Consultancy	02	01
Total	63	48

### **3. FAIDAZA MRADI**

#### **3.1 FAIDA ZA WAKATI WA UJENZI**

- Kuwepo kwa fursa za ajira
- Kukua kwa kipato cha wananchi maeneo ya mradi
- Kujengewa ujuzi kwa wote watakaoshiriki kwenye shughuli za ujenzi

#### **3.2 FAIDA ZA BAADA YA UJENZI**

- Kuboresha na kuongeza kiwango cha ubeabajji mizigo kwa miundombinu ya reli na madaraja.
- Kuongezeka kwa mwendokasi wa treni kutoka kilometra 30 kwa saa hadi kufikia kilometra 70 kwa saa na hivyo kupunguza gharama za safari na usafirishaji.
- Kupunguza muda wakupakia na kupakua mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam hadi bandari kavu ya Isaka kufikia saa 24.
- Kutengenezwa kwampango endelevu wamatengenezo ya miundombinu ili kufanya usafiri huu kuwa wauhakika na kuaminika.
- Kujengewa uwezo wafanyakazi wa reli na hivyo kuongeza ufanisi katika kutoa huduma.
- Kupunguza gharama za maisha.
- Kupunguza gharama za matengenezo ya barabara na hivyo serikali kuelekeza baje ti iliyookolewa kwenda kwenye huduma nyingine za kijamii.